Teacher.co.ke

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA NNE**

**KARATASI YA TATU, MUHULA WA PILI 2025**

## SEHEMU A: RIWAYA

**CLARA MOMANYI: Nguu za Jadi**

a. Mbinu za kimtindo

i. Nidaa/ siyali- majaani! Mama yangu!
ii. Balagha/ mbalagha/ swali butu- mrima amefikia kiwango hicho
iii. Taswira mghuso- machozi yalianza kumtiririka.
iv. Tashbihi- aliketi chini akalia kama mtoto mdogo.
v. Majazi- Majaani- pahali pa marundo ya taka.

b. Umuhimu wa mandhari ya dondoo (zozote sita)
i. Yanatusaidia kuelewa kina cha ukengeushi wa Mrima
ii. Yanatusaidia kuelewa madhara ya uraibu wa kuleo na dawa za kulevya.
iii. Yanatusaidia kuelewa jinsi Mbungulu alivyotumika kujenga mtiririko wa vitushi
iv. Yanatusaidia kuelewa ujasiri wa Mangwasha
v. Yanatusaidia kuelewa uozo katika jamii (Majaani kuna wauaji wa wachopozi)
vi. Yanatusaidia kuelewa maudhui ya utabaka (wasakatonge wanazumbua viziki Maajani) (zozote 4 x 1)

c) Maudhui matatu yanayodhihirika

i. Ukengeushi- Mrima alihamia majaani – mtaa wa wahauri
ii. Mabadiliko- Mrima anabadilika kutoka kijana mtanashati aliyeaminika na kuhamia mtaa wa Majaani.
iii. Madhara ya ulevi na mihadarati- ulevi unamfanya Mrima atekeleze familia yake.
iv. Umaskini – wasakatonge wanazumbua riziki Majaani -eneo la marundo ya (zozote 3 x 1= 3)

d) Umuhimu wa Mbungulu kulingana na dondoo



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

i. Ametumika kuchimuza baadhi ya sifa za Mangwasha ( mwenye mapenzi ya dhati- analia anaparifiwa hali ya Mrima.
ii. Ametumika kujenga mtiririko wa vitushi- anagundua ulipo Mrima -Majaani (zozote 2 x 1= 2)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

e) Hulka au sifa za Mrima

i. Mwenye bidi- alikuwa wa kwanza kufika afisini na wa mwisho kuondoka.
ii. Mlevi- anapotelea mtaa wa Pondo Mali kunywa vileo.
iii. Mwenye mapuuza- anatekeleza familia yake
iv. Mjinga- anapotoshwa na Sagilu
v. Mbinafsi – anapokea kutoka kwa Sagilu Kwenda kujistarehesha Ponda Mali
vi. Msikivu- aliskiliza ushauri wa akina lonare arudi nyumbani
vii. Mbabedume- anashikilia mila zinazompa mume nafasi kuliko mwanamke- asema aweza kuoa idadi yoyote ya wanawake.
viii. Mhafidhina/mtamaduni- anachelea kurudi nyumbani Kwenda kutunzwa kama mtoto.
ix. Mzinifu- ana uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa
x. Saliti- anawasalitu wanawe na mkewe kwa kuwatelekeza
xi. Kigeugeu- anawacha pombe kwa juma moja kisha anarudia tabia hiyo. (zozote 6 x 1= 6)

**SEHEMU YA B: Tamthilia ya Bembea ya Maisha: T. Arege**
***Jibu swali la 2 au 3***
**2.** "Bidii anayo lakini hana murua"
**a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)**
i. Msemaji wa amneno haya ni Asna.
ii. Anazungumza na Sara.
iii. Wako hospitalini, mjini.
iv. Asna anasema haya akimjibu Sara aliyekuwa anamtetea Bunju kuwa n mchapakazi. Asna ana mtazamo kinyume.
**Zozote 4x1=4**

**b) Eleza sifa za mrejelewa katika dondoo hili. (alama 4)**
**Mrejelewa ni Bunju-sifa zake**
i.Mwepesi wa kukasirika – msimamo wa Neema kuwa Lemi alizoa alama nzuri lakini akachukua nafasi ya ishirini unamkasirisha Bunju. Anasema, "Eti alama! My foot!"
ii. Msema kweli – Neema anapowomba amtilie pondo mama mkwe aende akaangaliwe na daktari, Bunju anamwambia wazi kuwa ana majukumu mengi.
iii. Mwajibikaji – Bunju ananunua sukari pamoja na mavazi kwa familia. Aidha, anaomba mkopo wa benki ili kujengea nyumba.
*iv.* Mwenye msimamo thabiti–Neema anapomshawishi kuhusu mila, Bunju anasema hata wakalijadili hilo siku nzima, maneno hayo hayatamwingia. Anashikilia msimamo kuwa hawezi kuacha ay a kuvuta riziki aende michezoni(ampeleke Lemi *out).*



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

v. Mwenye utamaduni–anamwambia Neema kuwa ay a a desturi hazimruhusu kukaa na wazazi wake maana hili lingeleta laana.
vi. Mwenye huruma – Neema anapohusika katika ajali, Bunju analipa gharama za hospitali. Anaita *Flying doctors* kwa msaada.
vii. Mwenye utu – anayafadhili masomo ya Salome kwa kumlipia karo ya shule ya upili ay a chuoni. **Zozote 4x1=4**

**c) Fafanua nafasi ya vijana kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha. (alama 12**
i. Vijana ni wasomi: Neema, Asna, Salome na Bunju wamesoma na kuhitimu vyuo vikuu. Kwa mfano, Neema ana digrii mbili kama anavyosema Asna.
ii. Vijana ni wenye bidii: Neema ni mchapa kazi sana.huondoka alfajiri na kurudi usiku watoto wakiwa wamelala. iii.
Vijana wana utu: Bunju anajitolea kugharamia matibabu ya Neema baada ya kuhusika kwenye ajali. Ikumbukwe kuwa ndiye aliyemfanyia Neema mpango wa kupata huduma ya dharura wa Flying Doctors lichaya kuwa Neema alikuwa mtu baki/asiyehusiana naye kwa damu.
iv. Vijana ni wawajibikaji: Bunju anawajibikia mahitaji ya chakula, mavazi, matibabu na karo ya wanawe. Anatekeleza wajibu wake kama mume, tena kikamilifu.
v. Vijana ni wanamageuzi/wanamapinduzi: Kupitia ushauri wa Sara, Neema anajitolea kubadilisha
mtazamo wa wanajamii kwa mfano anakubali kutumia vishawishi badala na kukabiliana na babake, Yona.
vi. Wanamaendelea: Luka anasifia maendeleo ya wasichana wa Yona. Anasema kuwa wameleta mwanga kijijini.
vii. Wazindushi: Neema na Asna wanajaribu sana kumzindua mama yao/Sara kutambua kuwa si tatizo yeye akilala kwa Bunju kwani mila hiyo si muhimu katika kizazi cha sasa.
viii. Walaza-damu/wazembe: Asna anakiri kuwa yeye hapendi kupika. Anamwambia mama yake kuwa wakti mwingine hulazimika kula makte na chai ya mkandaa.
ix. Wakengeushi: Asna anakengeuka na kukiri kuwa yeye hataki kuzungushwa kichwa na mwanaume. Hataki kabisa kujiingiza katika ndoa kwa sasa licha ya vishawishi vya mama yake.
x. Vijana ni wenye tuhuma: Asna anamtuhumu Bunju kuwa ni bahili, mwenye moyo mgumu kama jiwe na mkono wa birika. Hili si kweli kwani vitendo vya hisani ya Bunju yanaashiria kinyume.
xi. Vijana ni werevu: Wasichana wa Yona wana akili kama sumaku. Sara anasema kuwa hizo ni akili za kwao. Yona vile vile anadai kuwa akili zake ndizo sumaku haswa!
xii. Vijana ni wabishi/wagombanifu: Neema anazua majdala mkali baina yake na mumeweBunju kuhusu swala la mamake Neema kulala kwao na swala la Bunju kumpiga jeki Neeema katika matibabu ya Sara. Bunju naye anaendelea na ubishi kwa muda.
xiii. Vijana wana mapenzi ya dhati: Mapenzi ya Asna na Neema kwa mama yao ni wazi. Neema anagharamia matibabu ya hospitali. Asna anampa hifadhi kila allipoenda hospitali mjini. Wanazungumza na kwa muda tena kwa mlahaka mzuri wakati mwingine wakishauriwa na mama yao.
xiv. Vijana wanatelekeza majukumu ya malezi: Watoto wa Neema hawana muda wa kukaa na kulelewa na mama yao. Neema anakiri kuwa anashindwa kazini mpaka usiku na mtoto anamwona tu akiwa kitandani. Ikumbukwe kuwa watoto hao hawajui hata neno moja la lugha yao asili kama anavyolalamika babau yao, Yona.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xv. Vijana ni wababedume: Bunju analalamika kuwa mkewe Neema anampangia kazi za ndani na hata kumpangia kumpeleka mtoto/Lemi michezoni. Hili analiona kuwa si sawa kwa mume kufanya.
xvi. Vijana ni watamaduni: Yona anasisitiza kuwa Sara (mama mkwe) hawezi kulala kwake, ni laana.Anamweleza Neema hata wazazi wake walipkuwa hai hawakuwahi kulala kwake.

**Zozote 12x1=12**

**3.a)**

i. Uzungumzi nafsia . Mfano. Neema anajisemea maneno haya baada ya kutoka nje.
ii. Matumizi ya sentensi fupi.Mfano. Bunju ni mmoja went.
iii. Mlinganisho. Mfano. Wakati huo sikuona sasa ninaona.
iv. Tanakuzi. Mfano. Wakati huo ni tanakuzi ya sasa.
v. Methali. Mfano. Mwenye macho haambiwi tazama.
vi. Nidaa. Mfano. Kweli ulioje! Hebu fikiri!
vii. Kinaya. Mfano. Neema wakati mwingine hulalamika kuhusu Bunju ilhali anafahamu yeye ni zawadi kwao.
viii. Mbinu rejeshi. Mfano. Neema kukumbuka tendo la awali.
ix. Sitiari. Mfano. Bunju ni zawadi nzuri kwetu.
x. Swali balagha. Mfano. Mtu huyu atakosaje kuwa zawadi kwako?
xi. Msemo.Mfano. Maji yamezidi unga.
xii. Usambamba. Mfano. Usingepikika usingelika.
xiii. Mdokezo. Mfano. Hebu fikiri...umepata.
xiv. Kuchanganya ndimi. Mfano. flying doctors.
xv. Tashihisi. Mfano. ndege inafika.
xvi. Chuku. Mfano. ninakwambia kila kitu...analipia kila kitu.
xvii. Nahau. Mfano. achwa mahututi...
xviii. Taswira. Mfano. anaguswa. (16×1)

b). Toni ya huzuni. Mfano. Neema anajisemea maneno haya kwa huzuni akikumbuka jinsi kisa cha ajali yake kilivyokuwa na jinsi alivyosaidiwa. (2x1)

Ch). Maudhui yanayojitokeza ni:

i. Utu. Mfano. Neema anarejelea kitendo cha hisani na msaada aliopewa na Bunju.

ii. Usamaria mwema. Mfano. Bunju anamwokoa majeruhi wa ajali.(2×2)

**4a.** Aina za taswira



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

i. Taswira hisi. Mfano. hilo la mtoto kulala lilinigusa.

ii. Taswira oni. Mfano. nilikata simu na kutazama saa.

iii. Taswira mwendo. Mfano. na kuelekea maegeshoni.

iv. Taswira mguso. Mfano. nikaufungua mlango. (4×1)

**b.** Aina ya nafsi.

i. Nafsi ya kwanza.k.v. nilikata simu.

ii. Njeo iliyopita. k.v. ulinigusa. (2×1)

**Ch.** Mbinu za kimtindo

i. Usambamba .k.v. nilikata....nilizima....nikafungua

ii. Nidaa. k.v. saa nne kasorobo!

iii. Tashihisi. k.v. hilo la mtoto kulala lilinigusa.

iv. Usimulizi. k.v. nilikata simu, niliximа.... (4×1)

**d.i.** Kuitishwa chakula na mtoto wake Mercy ilhali hana hicho chakula.

ii. Mkewe kulala chumba kimoja naye ilhali hajala.

iii. Anaguswa na hali kuwa mkewe anamrejelea kwa jina like halisi.

iv. Msimulizi anaguswa na hali ya kutolipwa mshahara.

v. Msimulizi anaguswa na hali kuwa hajampihia mamake simu licha ya kuahidi kumpigia akifika nyumbani.

vi. Hali ya kuwa mkewe amekuja likizo ya wiki mbili kumtembelea ila hajapata wakati wa kukaa naye nyumbani.

vii. Hali kama Vaite atakubali kumkopesha unga wa kuukimu familia yake.

Viii. Mkewe haelewi kuwa hajalipwa mshahara wa miezi miwili.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ix. Mkewe kumtaka aandamane na mtoto kazini kwa sababu nyumbani hakuna chakula.

x. Mamake anamtaka atume pesa za kumlipa fundi ambaye malipo yake yamechelewa karibu mwezi mzima. (5×2)

**5.**Maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii

a. i) Toba ya kalia

i. Vijana wamechorwa kama wasomi- Jack na Siri walisomea katika shule ya Upili ya Kayole.
ii. Vijana wamesawiriwa kama wenye bidi- Jack alikuwa na mradi bora zaidi katika mashindano ya somo la Sayansi.
iii. Ni wasaliti – Siri alimsalitu Jack kwa kumhini ushindi wake.
iv. Mi wasamehevu- Jack anaisamehe familia ya Bwana Kalia na Bi Mshewa.
v. Ni wenye utu- Siri anatoboa siri ya namna walivyomhini Jack.

b. Ahadi ni Deni

i. Vijana ni wasomi- Fadhumo alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili wakati wazazi wake waliaga.
ii. Ni walezi wema- Fadhumo anawalea wanuna wake
iii. Wenye msimamo thabiti- Fadhumo alikataa kuwa kimada wa jamaa wa familia ya babake.
iv. Si wawajibikaji- Mwalimu aliomba wasichana wote wangalikuwa kama Fadhumo kwa bidi na utiifu
v. Vijana ni wakakamavu- Fadhumo anarejelea masomo baada ya miaka sita.

c. Nilitamani

i. Vijana ni wenye matumaini- Tumaini aliguria Tanzania kutoka Kenya kusaka maisha mema.
ii. Ni wenye utu- Nina alimhifadhi Tumaini
iii. Wenye tamaa- Tumaini alimpenda Romeo kwa utanashati
iv. Wenye mapuuza – Tumaini alipuuza ushauri wa Nina juu ya Wabongo
v. Wenye wivu- Tumaini alimwonea Nina wivu kwa kuwa na mume mzuri.
vi. Mpenda anasa- msimulizi anasema maisha ni kuishi leo, wa kesho aishile?



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

d.Pupa

i. Mpenda anasa- Mwakuona anatamani vyakula ainaina.
ii. Mwepesi wa kudanganya- Mwakuona anapoarifiwa anatafutiwa pasipoti anasalitika.
iii. Mwasherati- pale chenga – ways wasichana waliovalia nusu uchi walitembea kwa madaha.
iv. Adui wa wenzao- Mwakuona anachekelewa na vijana wengine wa kike waliotekwa nyara na kutunukishwa katika Chenga-ways
v. Chombo cha burudani- akina Mwakuona wanachaguliwa na wanaume Chenga-ways kujiburudisha
vi. Mwenye tamaa- Mwakuona alitamani vyakula kama pizza, nguo za bei, n.k.

(zozote 5 x4 = 20)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**
**a)**
**Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili.**
**(alama 5)**
i. Siku kuu mwenyenzi Mungu anaimbiwa nyimbo.
ii. Wengine hula mibofu siku hiyo.
iii. Siku kuu hufai kuingia katika anasa.
iv. Hufai kuwa mlafi wakati wa siku kuu.
v. Ni vyema kukwepa balaa.
vi. Ni mhimu kuzingatia maadili wakati wa siku kuu.
vii. Ulofa haufai kuwepo wakati wa siku kuu.
viii. Ni vyema kuepuka ukupe
ix. Vijana waepuke vurumai wakati wa siku kuu.

**Zozote 5x1=5**

b) Ukitumia vina vya shairi hili, liweke shairi hili **katika bahari inayofaa**.
(alama 2)
Ukaraguni-kila ubeti unajitegemea kivina./kila ubeti unatofautina na mwingine kivina.
**1x2=2**

**c) Andika ubeti wa kwanza katika lugha ya nathari.**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**(alama 4)**
Siku kuu iliyongojewa sana imefika. Mungu anaimbiwa nyimbo za sifa kwa raha. Watu wanafaa kufurahia siku hii kwa chakula kizuri kama vile minofu. Vijana nawaomba msiwe na anasa wakati wa siku kuu.
**Zozote 4x1=**

**d) Onyesha uhuru wa kishairi ulivyotumiwa na mshairi.**
**(alama 2)**
i. Inksari- asosikia-asiyesikia, aloona-anayoona
ii. Kuboranga sarufi-nyimbo mola kumwimbiya
**Zozote 2x1=2**

**e) Huku ukitoa mifano, onyesha matumizi manne ya mbinu za lugha zilizotumiwa.**
**(alama2)**
i. Takririri-vijana
ii. Tashbihi-naondoka kama tai
iii. Jazanda-nakuweka mwangazani
**Zozote 2x1=2**
**f) Eleza kanuni za utunzi zilizotumiwa katika ubeti wa nne.**
**(alama 4)**
i. Urari wa vina-kwa mfano vya ndani ni ta,ta,ta,ri, na vile a, a, a, jo.
ii. Kuna urari wa mizani-8,8
iii. Kuna urari wa vipande-viwili katika kila mshororo.
iv. Kuna utoshelezi wa ujumbe katika ubeti huu.
**Zozote 4x1=4**

g) Tambua toni katika shairi hili.
Himizo/kushauri/kuasa (alama 1)
**1x1=1**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**
**a) Huku ukitoa mifano, toa ithibati kuwa hili ni shairi huru (alama 5)**
i. Idadi ya mishororo hailingani-kwa mfano ubeti wa 5 una mishoror mitano ilhali beti zingine zina mishororo sita
ii. Idadi ya mizani inatofautiana katika kila mshororo-kwa mfano mshororo wa kwanza ubeti wa kwanza una silabi 2 ilhali wa pili una mizani 4.
iii. Mpangilio vina hauna usawa/hakuna urari wa vina -kwa mfano ubeti wa kwanza ti,ke, ngu, si na ki.
iv. Lina mishata-mishororo isiyokuwa kamili-mshororo wa kwanza katika beti za kwanza nne
v. Kuna urudiaji mwingi wa maneno-maendeleo.
**Zozote 5x1=5**

**b) Mtunzi wa shairi hili alidhamiria nini? (alama 1)**
Kueleza mambo yanayodidimiza maendeleo/kueleza maana ya maendeleo.
**Zozote 1x1=4**

**c) Bainisha matumizi mawili ya mbinu za kimtindo katika shairi hili. (alama 2)**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

i. Takriri-maendelea ya umma
ii. Nidaa la!
**Zozote 2x1=2**

**d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya kawaida. (alama 4)**
Maendeleo ya umma ni vitu kumilikiwa na wanyonge kupewa kwa bei ambayo wanaweza kumudu bila kuwadhulumu wala kuwadanganya kwani hiyo ndiyo haki.
**4x1=4**

e) **Eleza mambo yanayodhihirisha kuwa nchi imepiga hatua kiuchumi kwa mujibu wa shairi hili.**
(alama 4)
i. Wanyonge kupewa vitu kwa bei nafuu bila kudhulumiwa wala kudanganywa
ii. Dola inapodhibiti kila kitu kilichoagizwa nchini
iii. Watu kuhusishwa/ kuruhusiwa kutoa maoni katika shughuli bila udikteta
iv. Kuwepo kwa usawa wa watu wote.
**Zozote 4x1=4**

**f) Eleza kwa kutoa mfano mbinu ambayo mtunzi wa shairi hili ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa sita. (alama 2)**
Kuboronga sarufi-katika zao shughuli badala ya katika shughuli zao.
**Zozote 1x2=2**

**g) Eleza aina ya urudiaji unaojitokeza katika ubeti wa pili na uonyeshe umuhimu wake katika shairi hili. (alama 2)**
Urudiaji wa silabi-tu
Huleta mdundo fulani wa kimziki shairi linapokaririwa.
**Zozote 2x1=2**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**8.a)** Mbinu za kuhifadhi fasihi simulizi

i. Katika akila ya binadamu.

ii. Maumbile na mazingira. k.v. fisi kuchechemea.

iii. Katika vifaa meme. k.v. video.

iv. Katika michoro. (3×1)

II. Aina za vitendawili.

i. Sahili. k.v. vitendawili vinavyoundwa kwa maneno machache.

ii. Tata. k.v. huwa ni fumbo linalohitaji kuchemsha bongo ili kung'amua jawabu.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

iii. Simulizi. k.v. husimulia hadithi kama msingi wa kitendawili.

iv. Tanakali.k.v. huundwa kwa maneno yanayoiga sauti inayotolewa na kitendo k.m. Chururu si ndo! ndo!ndo!

v. Mkufu. k.v. huwa sehemu zinazohusiana na kuchangiana kimaana na vina urefu fulani. (3×1)

III. Matumizi ya lugha katika vitendawili.

i.Taswira. k.m. kuku wangu kategs mwibani.(nanasi)

ii. Sitiari. k.m. Nyumba yangu haina mlango.(yai)

iii. Kejeli.k.m. Uzi mwembamba umefunga dume kubwa.(usingizi)

iv. Tashihisi. k.m. Popote niendapo amenifuata. (kivuli) (3×1)

B. i. Ngomezi....ni fasihi ya ngoma.

ii. Ujumbe uliowasilishwa na ngomezi.

a. Kuzaliwa kwa mtoto.

b. Ndoa.

Ch.. Kifo.

d. Uwindaji.

e. Vita vya ukabila.

f. Majulio ya mvua.

g. Kuwaita kwa mchezo wa mleleka.

h. Kuwaita watu kwa jambo la dharura. (3×1)

III. Sifa za ngomezi.

a. Si rahisi kupata ujumbe wa ngomezi kama wewe si mshiriki wa utamaduni husika.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

b. Ngoma ni muhimu kupitisha ujumbe.

Ch. Wanajamii tu ndio wanaoweza kufasiri mdundo wa ngoma.

d. Ujumbe wa dharura huwasilishwa kwa njia ambayo si ghali ikilinganishwa na njia nyingine.

e. Mapigo yaliyotolewa kwa maana maalum huambatana na ngoma inayoeleweka kwa ujumbe mahususi.

f. Huongozwa na watu teule katika jamii. (4×1)

IV. Mifano ya ngomezi.

i. Milio ya ambulensi.

ii. Milio ya magari ya polisi.

iii. Ving'ora.

iv. Kengele( shuleni, kanisani na mahakamani)

v. Toni za kengele za simu.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes